JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

Tarehe: 19/08/2021

TANGAZO LA ZABUNI YA UJENZI

TANGAZO LA ZABUNI YA UJENZI WA WODI TATU KATIKA HOSPITAL YA WILAYA BUHIGWE.

1. Halmashauri ya wilaya Buhigwe imepokea fedha kutoka **Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**,Kwa ajili ya kulipia gharama za Mpango wa kazi ya ujenzi wa Wodi Tatu katika hospitali ya wilaya ya buhigwe,.Hivyo Halmashauri hapa ifahamike kama taasisi Nunuzi(TN) inakusudia kutumia sehemu ya fedha hizi kwa mchakato wa kulipia gharama za ujenzi kwa mkataba wa mafundi wa kawaida(LOCAL FUNDI) na wala si kandarasi.

2. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya Buhigwe Inapenda kuwakaribisha mafundi ujenzi(uashi) wakuu wanaostahili kuwa na sifa za ujenzi (uashi) na ambao wao wenyewe wataajiri mafundi uashi wasaidizi ,upauaji na kazi zingine zote zihusianazo na kukamilika kwa ujenzi wa zabuni tajwa hapa chini:

I. ZABUNI YA UJENZI WA WODI 3 ZA HOSPITAL YA WILAYA.

A. KIPANDE A: WODI YA KWANZA (MAMA)
NAMBA YA ZABUNI:LGA/138/BHDC/UJ/HSP/W1/2021-2022/01.

B. KIPANDE B: WODI YA PILI (WATOTO)
NAMBA YA ZABUNI: LGA/138/BHDC/UJ/HSP/W2/2021-2022/01.

C. KIPANDE C: WODI YA TATU (WABABA)
NAMBA YA ZABUNI:LGA/138/BHDC/UJ/HSP/W3/2021-2022/01.

II. Mchakato wa Zabuni hii ya ujenzi ni wa fundi mkuu mtaalamu wa ujenzi unaoshindanishwa kwa uwezo, haki,usawa, uwazi na gharama nafuu ya mafundi wataalamu wa uashi (LOCAL FUNDI MKUU) wa Kitanzania tu. Kwa yeyote atakayeweza kuona kwenye mbao za matangazo, ila Halmashauri itapendelea zaidi kupata fundi wakuu kutoka wilaya za Mkoa wa Kigoma Kwa ajili ya kuendana na

gharama za maandalizi ikiwa ni pamoja na muda kuwa muhimu kuuzingatia (Mobilization and Time factor Cost)

4. Tangazo hili pamoja na kwamba ni la local fundi lakini linazingatia sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016 pamoja na kanuni zake za manunuzi ya umma ya mwaka 2013;GN Na. 446 inayohusu manunuzi ya bidhaa (B) Goods) Ujenzi (uj) works) na huduma zisizo za ushauri wa kitaalamu na taaluma (H) Non -consultance services) na mauzo yote ya mali za umma kwa kupitia mnada (Disposal of public asset by Tender/Auction). Ambapo mtu anayetimiza vigezo vyote ndipo anafikiriwa gharama ya mkataba wa ujenzi ambayo ni ya chini kuliko wengine ndiye anayestahili yaani Eligibility ndio inayohusika zaidi.

MASHARTI YA ZABUNI

MWENYE NIA YA KUINGIA KWENYE KINYANG'ANYIRO HIKI CHA USHINDANI MDOGO (MIN COMPETITION)NI MUHIMU AWE NA SIFA ZIFUATAZO ILI AONEKANE KUFAA KUOMBA KAZI HII.

1. AWE NA UZOEFU WA UFUNDI UJENZI NA AWEZE KUITAFSIRI RAMANI VIZURI ILI APATE GHARAMA ZA VIFAA HIVYO NA ZA UFUNDI (LABOUR CHARGES) PIA AAMBATANISHE NA NYARAKA ZA UZOEFU PAMOJA NA MAOMBI YAKE HUSIKA YA ZABUNI HII.

2. MAOMBI YAONYESHE WAZI WAZI MCHANGANUO WA HATUA ZA UJENZI MZIMA YAANI KUANZA KWA UJENZI WA MSINGI, UKUTA, UPAUAJI, UMALIZIAJI WOTE NA SHUGHULI ZINGINE ZA UJENZI MPAKA MWISHO WA KUMALIZA UJENZI NA MAKABIDHIANO. RAMANI ZINAPATIKANA OFISI YA MANUNUZI HALMASHAURI YA BUHIGWE.

3. TAMKO LA KUTOKUWA NA MIGOGORO YOYOTE YA HAPO AWALI (NYUMA) NA HATA SASA KATIKA KAZI ZAKE ALIZO WAHI KUFANYA NA ANAZOFANYA HIVI SASA NA KAMA ANAKAZI NYINGINE KAMA HII BASI IWE KATIKA HATUA YA ASILIMIA (70%) KUMALIZIKA.

4. AKUBALI KUWA KATIBU TAWALA WILAYA NDIYE ATAKAYE KUWA MSULUHISHI WA MWANZO ENDAPO PATAKUWA NA MIGOGORO YA KIUTEKELEZAJI WA MRADI HUU. KABLA MIGOGORO HAIJAFIKIA HATUA ZA MBELE ZA KISHERIA.

5. TAMKO LA KUTOJIHUSISHA KABISA NA RUSHWA NA/AU UPOTOFU WA TAARIFA ZAKE (UDANGANYIFU).

6. TAMKO LA ULINZI NA USALAMA WA AFYA NA MAZINGIRA KWA WAFANYAKAZI WAKE NA WATU JIRANI NA UTEKELEZAJI WA MRADI NA MAZINGIRA YANAYOZUNGUKA MRADI.

7. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA **MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE, S.L.P 443, BUHIGWE;**NA KUTAJA JINA NA NAMBA YA ZABUNI PAMOJA NA KIPANDE ATAKACHO CHUKUA KWA AJILI YA UJENZI HUU.ILI MKATABA UWE NA NGUVU AWE NA TAMKO LA NGUVU YA KISHERIA YA KUJIWAKILISHA YEYE MWENYEWE KAMA NDIYE FUNDI MKUU YAWASILISHWE KWA MKONO NA YATAPOKELEWA KWENYE OFISI YA KATIBU WA BODI YA ZABUNI KWA NIABA YA MKURUGENZI MJENDAJI NA KAMATI YA UJENZI YA MRADI HUSIKA NA TAASISI NUNUZI(TN).NA **MWISHO WA MAOMBI HAYA NI TAREHE ...01/09/2021**..... SIKU YA JUMATANO....., SAA 7:30 **MCHANA** NA YATAFUNGULIWA HAPO HAPO SAA HIYO MBELE YA WAJENZI WAKUU MCHANA HUO.WOTE WALIOOMBA NA/AU WAKIWEPO WAWAKILISHI WAO UFUNGUZI UTAKUWA KWENYE **OFISI YA MANUNUZI NA UGAVI** MARA TU BAADA YA KUFUNGA UPOKEAJI.

8. HALMASHAURI HAITAPOKEA MAOMBI YOYOTE YALIYOCHELEWA AU KUTUMWA KWA NJIA NYINGINE YOYOTE NA HATA YAKIPOKELEWA MAOMBI HAYO HAYATAFUNGULIWA BALI YATARUDISHWA.

9. MAOMBI YAWE NA NAKALA HALISI MOJA (1) NA **NAKALA KIVULI MBILI (2)** NA VIAMBATANISHI VYAKE VYOTE ZIWEKWE KWENYE BAHASHA TATU TOFAUTI ZIKIANDIKWA HALISI NA VIVULI. KWA MBELE ZIANDIKWE ANWANI YA HALMASHAURI KAMA ILIVYOELEKEZWA KIPENGELE CHA 7 NA NYUMA YA BAHASHA HII IANDIKWE ANWANI YA FUNDI MKUU. HIZI NI BAHASHA ZA NDANI NA HALAFU ZIWEKWE KWENYE BAHASHA MOJA YA NJE YENYE ANWANI MBELE TU AMBAYO NI ANUANI YA HALMASHAURI.

TANGAZO LIMETOLEWA NA:

.....

Marycelina C. Mbehoma

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE